

# KARIBU ALBUQUERQUE!

## MWONGOZO WA MISAADA KWA WAHAMIAJI NA WAKIMBIZI

**Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi**

**Nambari ya simu: 505-768-3040 Barua pepe: OIRA@cabq.gov**

**1 Civic Plaza NW Floor 4th room 4072, Albuquerque NM 87102**

OEI immigrant & refugee affairs ABQ

# Jiji la Albuquerque linakukaribisha!

Jiji la Albuquerque lina mandhari ya kupendeza ya Milima ya Sandia, sherehe za kuvutia na vyakula vitamu maarufu. Zaidi ya hayo, wahamiaji na wakimbizi huchagua jiji la Albuquerque kama makao yao mapya kwa sababu ya hali ya anga ya jua ya kupendeza, upendo wa watu na hali ya ukarimu ya wenyeji wake

Lengo la mwongozo huu wa misaada kwa wahamiaji na wakimbizi ni kukaribisha wote wanaokuja na kushiriki maelezo ya kusaidia kuwezesha jamii hizi kuzoea maisha ya jiji la Albuquerque.

## Maadili ya Jiji la Albuquerque

### Kujitahidi kufanya Albuquerque kuwa jiji lenye usawa na bila ubaguzi!

Meya Tim Keller alianzisha Ofisi ya Usawa na Ujumuishwaji (OEI, Office of Equity and Inclusion) na Ofisi ya Haki za Raia (OCR, Office of Civil Rights) mnamo Machi 2018 ili kutekeleza maono yake ya kufanya jiji la Albuquerque kuwa jamii salama, bunifu na isiyo na ubaguzi kwetu sote. Dhamira ya Ofisi ya Usawa na Ujumuishwaji (Office of Equity and Inclusion) ni kutia msukumo na kuzipa idara zote za jiji maarifa na zana za kukubali na kutekeleza vipengele vya masuala ya utofauti, usawa na ujumuishwaji kama kanuni za msingi katika sekta zote za maisha ya umma.

Jiji la Albuquerque limeanzisha kanuni ya huduma za ukalimani ambayo inahitaji idara zote za Jiji kutoa huduma za lugha zinazohusiana na tafsiri na ukalimani kwa umma bila malipo. Ikiwa unahitaji huduma ya tafsiri au ukalimani ili kukusaidia kufikia huduma za jiji, tafadhali wasiliana na idara husika ya jiji ili kuomba huduma hizi.

Huduma za ukalimani

## Serikali ya Jiji la Albuquerque

Vifuatavyo ni vitengo vya serikali: Kitengo cha Sheria, Usimamizi Mkuu na Mahakama.

Anayeongoza kitengo cha Usimamizi Mkuu katika Jiji letu ni Meya Mayor Tim Keller. Baraza la Jiji ni kitengo cha sheria kinachosimamia Jiji la Albuquerque. Baraza hili kwa kawaida linafanya kazi kama kitengo cha sheria cha mtindo wa bunge au wajumbe, kupendekeza miswada ya sheria na kupitisha sheria za kusaidia kuongoza jiji. Baraza hili lina Madiwani 9 ambao huchaguliwa kwa mihula kila baada ya miaka 4. Unaweza kuwasiliana wakati wowote na ofisi ya Diwani na ofisi ya Meya ukiwa na maswali, wasiwasi au maoni yoyote.

Kitengo cha mahakama ni kitengo tofauti na huru cha serikali ambacho kinajumuisha Bernalillo County Metropolitan Court, Second Judicial District Court na United States Federal Court. Kwa maelezo zaidi nenda katika: Kuhusu Mahakama | Mahakama za New Mexico (nmcourts.gov)

## Sera Inayofaa Wahamiaji

Baraza la Jiji lilitangaza kwa mara ya kwanza jiji la Albuquerque kuwa Jiji Linalofaa kwa Wahamiaji mwaka wa 2000. Baraza lilipiga kura ili kuthibitisha upya hali yake ya kuunga mkono marekebisho ya kina ya uhamiaji mwaka wa 2015 na kwa wakimbizi wote mwaka wa 2017. Mwaka wa 2018, lilipitisha sera mpya, R-18-7, ambayo inaimarisha hali ya jiji la Albuquerque kama jiji linalofaa kwa wahamiaji. Sera hii mpya Inayofaa Wahamiaji ilianza kutekelezwa mnamo tarehe 24 Aprili 2018. Inakataza jiji kuuliza kuhusu hali ya uhamiaji ya mtu binafsi, uraia, mahali pa kuzaliwa au dini isipokuwa ili kubainisha ustahiki wa kushiriki kwenye mipango ya serikali au jimbo. Inakataza pia idara ya polisi kutekeleza sheria za uhamiaji za nchi. Azimio hii inaelekeza idara za Jiji kukagua sera, taratibu na desturi zote za sasa za Jiji ili kuhakikisha kuwa zinatii sera hii.

Kusudi la azimio hii ni kuendeleza usalama wa umma, kulinda haki za raia na kuheshimu hadhi ya wakazi wote huku ikiunda mazingira yanayofaa kwa waathiriwa wote wa makosa ya kikatili wanaotafuta msaada. Sera kamili inaweza kupatikana kwenye tovuti yetu hapa.

# Yaliyomo


Ofisi ya Mombo ya Wahamiaji na Wakimbizi....................4

Kamati Simamizi ya Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi....................5

Jua Haki zako.................... 6

Nambari za Simu za Huduma ya Dharura.................... 7

Watoa Huduma za Ukalimani....................8

Nyenzo za Jiji.................... 9

Vituo vya Jamii.................... 9

Maeneo ya Kituo cha Wazee na Watu wa Umri Tofauti.................... 11

Huduma za utoaji wa makazi mapya.................... 11

Huduma za Sheria ....................13

Huduma za Afya.................... 14

Msaada wa chakula.................... 14

Msaada wa Umma.................... 14

Nyenzo za Tamaduni Mbalimbali na Tamaduni Nyingi………………………………………………….,…… 15

Mafunzo ya Kazi na Kuajiriwa……………………………………………………………………………………..…. 16

Elimu (Shule ya Chekechea hadi Darasa la 12 (K-12)) na Mafunzo ya ESL…………………………….. 17

Ugonjwa wa virusi vya korona – Nyenzo………………………………………………………………………….. 19

Nyenzo za Ziada…………………………………………………………………………………………………………….20

## Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi (OIRA, Office of Immigrant and Refugee Affairs)




Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi (OIRA, Office of Immigrant and Refugee Affairs) ilianzishwa mwaka wa 2016 kwa msaada wa kampuni ya W.K. Kellogg Foundation, ili kupanga juhudi za kuhudumia vyema wakazi ambao ni wahamiaji na wakimbizi. OIRA ilijiunga na Ofisi ya Usawa na Ujumuishwaji (Office of Equity and Inclusion) mwaka wa 2018.

Dhamira ya Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi (Office of Immigrant and Refugee Affairs) ni kuboresha maisha ya wahamiaji na wakimbizi wote waliopata makazi mapya wanaoishi katika jiji la Albuquerque kwa kutambua na kushughulikia mahitaji yanayohusiana na huduma za afya, afya ya tabia, elimu, makazi, ajira na ukuaji wa uchumi.

Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi (Office of Immigrant and Refugee Affairs) iliunda kamati simamizi iliyojumuisha wafanyakazi kutoka kwa mashirika mbalimbali ya jamii yanayohudumia wahamiaji na wakimbizi.

OIRA iliamrisha kufanywa kwa utathmini wa kina wa mahitaji, nyenzo na utayari wa mipango na idara za serikali ya Jiji wa kujumuisha wahamiaji, wakimbizi na wanafunzi wa lugha ya Kiingereza katika jiji la Albuquerque. Utathmini, uliokamilishwa mwezi Julai 2017, ulibaini haja ya kuboreshwa kwa huduma za ukalimani kwenye huduma za Jiji na kwa huduma za uhamasishaji na usafiri ili kuboresha zaidi hali ya kushiriki kwa wahamiaji na wakimbizi katika sekta zote za raia. Utathmini huo pia ulibaini kuwa sera za kuendeleza usalama na ujumuishwaji wa wahamiaji na wakimbizi ni muhimu. Utathmini hii unatumiwa kama mwongozo na Ofisi ya Mombo ya Wahamiaji na Wakimbizi (Office of Immigrant and Refugee Affairs).

Sehemu za Kuzingatia:

- Kuboresha huduma za ukalimani kwenye huduma zote za umma na kutoa usaidizi wa kiufundi
- Kushirikiana na mashirika: shughuli na miradi inayohusiana na wahamiaji na wakimbizi
- Kutoa msaada wa mahitaji kutoka kwa idara za Jiji, mashirika na wanajamii
- Kushiriki nyenzo na mashirika ya jamii na wakazi.

## Ofisi ya Mambo ya Wahamiaji na Wakimbizi (Office of Immigrant and Refugee Affairs) Kamati Simamizi

**Madhumuni ya Kamati Simamizi ya OIRA ni**:

- Kuelekeza, kuwakilisha na kupigania mahitaji na maslahi ya wahamiaji na wakimbizi na kufanya serikali ya jiji kuwajibika kwa kutimiza mahitaji hayo.

**Majukumu ya Kamati Simamizi ni:**

- Kujulisha wawakilishi wa jiji kuhusu idadi ya wahamiaji na wakimbizi
- Kuhamasisha jamii kuhusu huduma za jiji zinazopatikana kwa jamii za wahamiaji na wakimbizi
- Kutathmini na kutoa kipaumbele kwa mipango, sera na miradi ambayo itashughulikia mahitaji ya wahamiaji na wakimbizi.
- Kutetea na kutoa mapendekezo ya sera na ugavi wa nyenzo zinazoshughulikia mahitaji ya wahamiaji na wakimbizi.
- Kuchunguza na kutathmini hatua zinazopigwa na serikali ya jiji ili kushughulikia mahitaji na maslahi ya wahamiaji na wakimbizi.




# Jua Haki zako

Kila mtu anayeishi Marekani ana haki za msingi chini ya katiba ya Marekani na chini ya sheria za haki za raia. Pata maelezo zaidi kuhusu haki zako, jinsi ya kuzitumia na hatua ya kuchukua wakati ambapo haki zako zimevunjwa.

### Nambari za Huduma ya Dharura/Programu

- Nambari ya Huduma ya Dharura ya United We Dream: 1-844-363-1423
- United We DreamProgramu ya Notificaili kukusaidia kujitayarisha kutokana na kufukuzwa nchini

### Rasilimali za Eneo

- ACLU New Mexico American Civil Liberties Union
- El Centro de Igualdad y Derechos (505) 246-1627
- New Mexico Immigrant Law Center
- New Mexico Faith Coalition for Immigrant Justice

### Jua Nyenzo za Haki Zako

- Mhamiaji Mwenye Ufahamu: Jua Haki Zako
- Vijitabu vya Jua Haki Zako vya Mradi wa Ulinzi wa Wahamiaji kwa lugha ya Kiingereza au Kihispania
- United We Dream Jua Uwezo Wako, Jua Haki Zako
- CLINIC: Jua Haki Zako

### Mfumo wa Kutambua Mfungwa wa ICE (ICE Detainee Locator)

- Mfumo wa Kutambua Mfungwa wa ICE (ICE Detainee Locator)

### Haki Wakati wa Mashambulizi

- Kituo cha Kitaifa cha Sheria za Wahamiaji (National Immigration Law Center) Haki za Nyumbani na Jua Haki Zako
- Kituo cha Nyenzo za Sheria za Wahamiaji (Immigrant Legal Resource Center) Red Cards
- ACLUMambo ya Kufanya Ikiwa Maajenti wa Uhamiaji (ICE) Wako Nyumbani Kwako na Video iko kwa lugha ya Kiingereza na Kihispania
- ACLU Mambo ya Kufanya Wakati Unashirikiana na ICE- Video kwa lugha 7
- American Federation of Teachers Mambo ya Kufanya na Kutofanya kwa wanafunzi ikiwa maafisa wa ICE wamekuja nyumbani kwao

## Nambari za Simu za Huduma ya Dharura

**Polisi/Moto/Dharura za Matibabu** **911**

**Huduma zisizo za dharura:** Kwa hali ambapo maisha, usalama au mali ya mtu binafsi haiko hatarini zaidi, lakini huduma ya usalama wa umma inahitajika 505-242-2677

**Kituo cha Mawasiliano cha Jamii cha Albuquerque cha 3-1-1** (3-1-1 ni njia rahisi ya kuwasiliana na Jiji ili kuripoti michoro, kelele za wanyama, kambi ya wasio na makao, matatizo ya kuchukuliwa kwa taka au mashimo barabarani) 311

**United Way** ........................................................................................................ 211 2-1-1 hutoa habari za bila malipo na rufaa za huduma za afya na binadamu, mashirika ya serikali na mashirika ya jamii.

**Huduma za Ulinzi wa Watu Wazima:** Huduma za Wazee na za Muda Mrefu za NM (NM Aging and Long-Term Services) (zinapatikana wakati wowote) * 1-866-654-3219

Ripoti madai ya dhuluma, utelekezaji au unyanyasaji wa watu wazima wenye umri wa miaka 18 na zaidi.

Huduma ya Gari la Wagonjwa la Albuquerque (inapatikana wakati wowote) * 505- 761-8200

**Idara ya Watoto, Vijana na Familia ya NM (NM Children Youth and Families Department (CYFD)** 1-855-333-7233
Huchunguza ripoti za madai ya dhuluma na utelekezaji wa watoto kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 18, na husimamia huduma ya malezi ya kambo na upangaji wa watoto, na mipango ya jimbo lote ya dhuluma za nyumbani. www.cyfd.org

**Kituo cha Maelezo ya Sumu na Dawa cha NM (NM Poison and Drug Information Center) (inapatikana wakati wowote) *** 1-800-222-1222 1650
University Blvd., NE, 87102 www.nmpoisoncenter.unm.eduWataalamu hutathmini na kutoa mapendekezo ya matibabu wakati wa matukio ya uwezekano wa kuathiriwa na sumu.

**Dharura za Huduma za Matumizi – Stima, Gesi na Maji**

**Stima** - Public Service Company of NM (PNM) (inapatikana wakati wowote)* 1-888-342-5766 4201
Edith Blvd., NE, 87107 www.pnm.com/report-an-outage 505-246-5700
Ripoti hali ya kupotea kwa stima au fahamu kuhusu hali ya kupotea kwa stima katika eneo lako.

**Gesi - NM Gas Company (inapatikana wakati wowote)*** 1-888-NM-GAS-CO au 1-888-664-2726 1625
Rio Bravo SW, Ste., 27, 87105 www.nmgco.comMaelezo ya usalama na dharura na kuripoti dharura zinazohusiana na gesi asili.

**Maji** - Albuquerque Water Utility Authority 505-842-9287
Chaguo la #1 Maswali ya Bili Chaguo la #0 www.abcwua.orgKituo cha usambazaji kinapatikana wakati wowote ili kuripoti dharura za maji na maji taka, kuomba kuzimwa kwa ajili ya dharura, kutoa huduma kwa wateja na kuripoti matumizi mabaya ya maji. Anwani: 1441 Mission Ave. NE, Albuquerque NM 87113

## Watoa Huduma za Ukalimani

**Valley Community Interpreters** 505-596-0592
Shirika la VCI hutoa huduma za lugha na maelekezo maalum ya wafanyakazi ili kukuruhusu kuwahudumia vyema wanajamii, wagonjwa na wateja wako.
https://www.vcinm.org/ Anwani: 400 Gold Ave. Suite 726 SW Albuquerque, NM 87102

**Todd-Reyes Interpreting and Translation** (505) 814-3327
Hutoa huduma za ukalimani wa lugha ya kisheria katika jimbo la New Mexico na eneo kubwa la Kusini Magharibi (Southwest). Tafsiri na ukalimani wa lugha ya

Kiingereza<>Kihispania kwa sekta za sheria, biashara, mashirika yasiyo ya faida, jamii na serikali https://certifiedlegalinterpreters.com/

**Babel Translation Services** 505-250-6155
nahid.haji@gmail.com Tafasiri na ukalimani wa lugha kama vile: Kiarabu, Kidari, Kifarsi, Kihindi, Kipashto, Kiswahili, Kiurdu

**United Voices for Newcomer Rights (UVNR)** (505) 277-0197
Tafsiri, ukalimani - Linazingatia zaidi kutoa huduma kwa jamii za wakimbizi. Kidari, Kipashto, Kiarabu, Kiswahili, Kinyarwanda, Kirundi, Kihispania, Kifaransa

# Nyenzo za Jiji

## Idara ya Huduma za Familia na Jamii ya Albuquerque

**Saa za Kazi za Kituo cha Huduma ya Afya na Jamii ni** Jumatatu hadi Ijumaa saa mbili asubuhi (8:00 am) hadi saa kumi na moja jioni (5:00 pm.) 505-768-2860

Vituo vyote hutoa msaada wa chakula cha dharura, huduma za matumizi na msaada wa kodi ya nyumba, msaada wa nepi za dharura, benki ya nguo (inapatikana katika vituo vya East Central na John Marshall). Unaweza kuhitaji kuweka miadi ili kupokea bidhaa za msaada maalum; wasiliana na vituo kwa maelezo zaidi.

Tovuti ya Vituo vya Afya na Jamii

**Kituo cha Huduma ya Afya na Jamii cha Alamosa** 505-836-8800 6900 Gonzales Rd., SW, 87121 Huhudumia wakazi wa maeneo ya Kusini Magharibi ya Mesa (South Valley na Westside) ya jiji la Albuquerque.

**Kituo cha Huduma ya Afya na Jamii cha East Central (East Central Health and Social Service Center)** 505-767-5700 7525 Zuni Rd., SE, 87108

Huhudumia wakazi wa maeneo ya Kaskazini Mashariki (Montgomery hadi Central na Tramway hadi Carlisle) na Kusini Mashariki (Gibson hadi Central na Tramway hadi Carlisle) ya jiji la Albuquerque.

**Kituo cha Huduma ya Afya na Jamii cha John Marshall (John Marshall Health and Social Service Center)** 505-848-1345 1500 Walter St., SE, 87102 Huhudumia wakazi wa eneo la Katikati mwa Jiji la Albuquerque (Central Albuquerque).

**Kituo cha Huduma ya Afya na Jamii cha Los Griegos (Los Griegos Health and Social Service Center)** 505-761-4050 1231 Candeleria Rd., NW, 87107 Huhudumia wakazi wa maeneo ya Northeast Heights, Northwest Valley na North Westside ya jiji la Albuquerque.

# Vituo vya Jamii

**Kituo cha Jamii cha Alamosa (Alamosa Community Center)** ...................................505-836-8760
6900 Gonzales Rd SW, 87121
**Kituo cha Jamii cha Barelas (Barelas Community Center)**......................................... 505- 848-1343
801 Barelas Rd SW, 87102
**Kituo cha Jamii cha Cesar Chavez (Cesar Chavez Community Center)**.................... 505-256-2680
7505 Kathryn Ave SE, 87108
**Kituo cha Jamii cha Dennis Chavez (Dennis Chavez Community Center)**.............. 505-848-1341
715 Kathryn Ave SE, 87102
**Kituo cha Jamii cha Don Newton - Taylor Ranch (Don Newton - Taylor Ranch Community Center)** ..........................................................................................................505-768-6006
4900 Kachina St NW, 87120
**Kituo cha Jamii cha Heights (Heights Community Center)**...................................... 505-848-1334
823 Buena Vista Dr SE, 87106
**Kituo cha Jamii cha Herman Sanchez (Herman Sanchez Community Center)**........ 505-848-1336
1830 William St SE. 87102
**Kituo cha Jamii cha Holiday Park (Holiday Park Community Center)**...................... 505-764-6425
11710 Comanche Rd NE, 87111
**Kituo cha Jamii cha Jack Candelaria (Jack Candelaria Community Center)**............ 505-848-1324
400 San Jose Ave SE, 87102
**Kituo cha Jamii cha Jeanne Bellamah ( Jeanne Bellamah Community Center)**........505-767-5910
11516 Summer Ave NE, 87112
**Kituo cha Jamii cha Joan Jones katika Atrisco Hills (Joan Jones Community Center at Atrisco Hills)** .........................................................................................................................505-836-8810
3828 Rincon Rd NW, 87105
**Kituo cha Jamii cha Johnny Tapia katika Wells Park (Johnny Tapia at Wells Park)** 505-848-1390
500 Mountain Rd NW, 87102
**Kituo cha Jamii cha Loma Linda (Loma Linda Community Center)**.......................... 505-764-1525
1700 Yale Blvd SE, 87106
**Kituo cha Jamii cha Los Duranes (Los Duranes Community Center)**........................ 505-767-5900
2920 Leopoldo Rd NW, 87104
**Kituo cha Jamii cha McKinley ( McKinley Community Center)**................................. 505-767-5930
3401 Monroe St NE, 87110
**Kituo cha Jamii cha Mesa Verde (Mesa Verde Community Center)** .........................505-767-5920
7900 Marquette Ave NE, 87108
**Kituo cha Jamii cha Singing Arrow (Singing Arrow Community Center)**.................. 505-291-6200
13001 Singing Arrow Ave SE, 87123

**Kituo cha Jamii cha Snow Park (Snow Park Community Center)**............................ 505-332-5250
9501 Indian School Rd NE, 87112
**Kituo cha Thomas Bell (Thomas Bell Community Center)**........................................505-848-1332
3001 University Blvd SE, 87106
**Kituo cha Jamii cha Mesa Magharibi (West Mesa Community Center)**................. 505-836-3487
5500 Glenrio Rd NW, 87105
**Kituo cha Jamii cha Westgate (Westgate Community Center)**................................ 505-836-8723
1400 Snow Vista Blvd SW, 87121
**Kituo cha Jamii cha Whittier (Whittier Community Center)**................................... 505-256-2093
1100 Quincy St SE, 87108

# Vituo vya Wazee na Watu wa Umri Tofauti

## Idara ya Masuala ya Wazee ya Jiji la Albuquerque/Wilaya ya Bernalillo

Shughuli za burudani, vyakula, fursa za masomo, huduma za jamii, uchunguzi wa afya na zaidi zinapatikana kwa watu wenye umri wa miaka 50 na zaidi.

Saa za kazi: Saa mbili asubuhi (8:00 A.M.) hadi saa kumi na moja jioni (5:00 P.M.), Jumatatu hadi Ijumaa; Saa za kazi za Jumamosi na jioni hutofautiana katika kila kituo. Piga simu kwa nambari 764-6400 ili ufahamishwe kuhusu ratiba iliyosasishwa au tutembelee mtandaoni: www.cabq.gov/seniors

**Kituo cha Wazee cha Barelas (Barelas Senior Center)** ...........................................505-764-6436
714 7th St., SW, 87102
**Kituo cha Wazee cha Bear Canyon (Bear Canyon Senior Center)**........................ 505-767-5959
4645 Pitt St., NE, 87111
**Kituo cha Wazee cha Highland (Highland Senior Center)**.......................................505-767-5210
131 Monroe St., NE, 87108
**Kituo cha Wazee cha Los Volcanes (Los Volcanes Senior Center)**........................ 505-767-5999
6500 Los Volcanes Rd. NW, 87107
**Kituo cha Wazee cha North Valley (North Valley Senior Center)**........................ 505-761-4025
3825 4th St., NW, 87107
**Kituo cha Wazee cha Palo Duro (Palo Duro Senior Center)**..................................505-888-8102
5221 Palo Duro Ave., NE, 87110

## Vituo vya Watu wa Umri Tofauti:

Vituo hivi viwili vinahudumia watu wenye umri wa miaka 6 na zaidi. Vituo vyote viwili hutoa huduma za burudani, huduma za jamii na fursa za masomo na nyingine nyingi. Saa za kazi: Saa

mbili asubuhi (8:00 A.M.) hadi saa tatu usiku (9:00 P.M.); Jumatatu hadi Ijumaa; Jumamosi, Saa tatu asubuhi (9:00 A.M.) hadi tisa alasiri (3:00 P.M.)

**Kituo cha Watu wa Umri Tofauti cha Manzano Mesa (Manzano Mesa Multigenerational Center)**………………………………………………………………………………………… 505-275-8731
501 Elizabeth St., SE, 87123
**Kituo cha Watu wa Umri Tofauti cha North Domingo Baca (North Domingo Baca Multigenerational Center)**…………………………………………………………………………505-764-6475
7521 Carmel Ave., NE, 87109

## Ofisi ya Usawa na Ujumuishwaji (Office of Equity and Inclusion) ya Jiji la Albuquerque

**Ofisi ya Masuala ya Wahamiaji na Wakimbizi (Office of Immigrant & Refugee Affairs)**
505-768-3040

Anwani: 1 Civic Plaza NW, Albuquerque NM 87102 Ghorofa ya 4 Chumba cha 4072

Tovuti ya Ofisi ya masuala ya wahamiaji na wakimbizi

## Huduma za Utoaji wa Makazi Mapya kwa Wakimbizi

**Lutheran Family Services (LFS)**ni shirika rasmi la utoaji wa makazi mapya kwa wakimbizi katika Jimbo la New Mexico. Shirika hili limejitolea kuwasaidia wakimbizi na wanaotafuta makao kuanza upya maisha yao kwa kuwawezesha kutimiza mahitaji yao ndani ya mwaka wao wa kwanza nchini Marekani na kuhimiza ujumuishwaji katika jamii zao mpya.

LFS lina Mipango ifuatayo inayopatikana: Mipango ya Ustawi wa Wamarekani Wageni (New American Pathways), Udhibiti wa Kina wa Hali (Intensive Case Management), Mipango ya Ajira ya Wakimbizi (Refugee Career Pathways), Mpango wa Waathiriwa wa Mateso (The Survivors of Torture Program), Mikopo ya Kulipia Kwanza Kabla ya Kupata Mkopo ya Uanzishaji wa Biashara Ndogo (Micro Enterprise Development Credit Builder Loans)

Tovuti ya Lutheran Family Services

Anwani: 230 Truman St NE, Albuquerque, NM 87108   Nambari ya simu: (505) 933-7032

**Shirika la Catholic Charities** lina  Kituo cha Msaada wa Wakimbizi ambacho hutoa mipango ya elimu na ajira kwa jamii nyingi za wakimbizi ambazo zimepata makazi mapya katika jiji la Albuquerque. Mpango huu unapatikana baada ya kukamilika kwa mpango wa utoaji wa makazi mapya wa siku 90 wa serikali ya Marekani. Mipango ya Shirika la Catholic Charities inalenga kuunda njia kwa familia na watu binafsi kushiriki katika jamii yao mpya kupitia elimu,

uwezeshwaji wa binafsi, fursa za uongozi, ushirikishaji wa jamii, kujiandaa kwa ajira na kutafuta uraia. [Tovuti ya Catholic Charities]

Anwani: 2010 Bridge Blvd SW, Albuquerque, NM 87105 Nambari ya simu: (505) 724-4670

**Shirika la ABQ Faithworks Collaborative**: Makundi ya dini ya jiji la Albuquerque yanayofanya kazi katika jamii ili kukaribisha wageni na kushughulikia mahitaji ya muda mfupi na ya kudumu ya wanaotafuta makao na watu wasio na makao. Mipango yao husaidia wakimbizi kujitahidi kutimiza mahitaji yao na kujumuishwa kwa wateja wao katika huduma za jamii za afya ya akili, mipango ya matibabu ya afya ya tabia, nyumba za bei nafuu, mafunzo ya kazi na msaada wa Kisheria.

[Tovuti ya ABQ Faithworks] Nambari ya simu: 505-457-1728 Barua pepe: info@abqfaithworks.org

# Huduma za Sheria

**Huduma za Uhamiaji na Uraia wa Marekani (USCIS, U.S. Citizenship and Immigration Services)** ni shirika la Serikali linalosimamia huduma ya uhamiaji halali nchini Marekani. Baadhi ya huduma wanazotoa zinajumuisha: Uraia (Inajumuisha mchakato husika wa kuwa raia kiasili), uhamiaji wa wanafamilia, kufanya kazi nchini Marekani, kuthibitisha Haki ya Kisheria ya Mtu Binafsi ya Kufanya Kazi Nchini Marekani (Uthibitishaji wa Mtandaoni (E-Verify)), mipango ya uhisani, upangaji, kujumuishwa kwa raia na elimu ya ukoo.

[Tovuti ya USCIS]

Nambari ya simu isiyolipishwa ni 800-375-5283 (TTY 800-767-1833). Saa za kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, saa mbili asubuhi (8 am) hadi saa mbili jioni (8 pm) Saa za Mashariki.

Ofisi za Eneo Husika: 1551 Mercantile Avenue NE Suite B, Albuquerque, NM 87107

**Kituo cha Sheria ya Wahamiaji cha New Mexico (NMILC, New Mexico Immigrant Law Center)**
Dhamira ya shirika hili ni kutekeleza haki na usawa kwa kuwezesha jamii za wakimbizi zenye mapato ya chini kupitia huduma shirikishi za kisheria, utetezi na elimu.

[Tovuti ya New Mexico Immigrant Law Center]

Anwani: 625 Silver Ave. SW, Ste. 410, Albuquerque, NM 87102 Nambari ya simu: (505) 247-1023

**Kituo cha New Mexico kuhusu Sheria na Umaskani (New Mexico Center on Law and Poverty)**

Dhamira ya shirika hili ni kutekeleza haki ya kiuchumi na kijamii kupitia: Elimu, Utetezi na Uwasilishaji wa Kesi Mahakamani. Tovuti ya NM for law and PovertyNambari ya simu: 505-255-2840

Anwani: 301 Edith Blvd NE, Albuquerque, NM 87102

### Ubalozi Mdogo wa Meksiko

Hutoa huduma nyingi kwa jamii ya Meksiko na wanajamii wengine kama vile hati za Meksiko, pasipoti, mada za uhamiaji zinazohusiana na wafungwa, elimu ya afya na fedha na nyenzo.

Tovuti ya Mexican ConsulateAnwani: 1610 4th St NW, Albuquerque, NM 87102

Nambari ya simu: 505-247-2147

## Huduma za Afya

**Mpango wa Afya ya Wakimbizi wa Idara ya Afya ya NM (NM Department of Health Refugee Health Program)** 505-841-8928 7525 Zuni SE, 87108 www.nmhealth.org/about/phd/idb/rhp/

Hushirikiana na mashirika mengine ya jamii ili kuwezesha ufikiaji wa huduma ya uchunguzi wa kimatibabu na huduma ya afya ya akili iliyojumuishwa kwa wakimbizi wageni.

## Msaada wa Chakula

**Echo Inc., Food** 505-242-6777
**Mpango wa Msaada wa Chakula cha Ziada kwa Wazee wa New Mexico (CSFP, New Mexico Commodity Supplemental Food Program for Seniors)**
300 Menaul NW, Chumba cha #226, 87107 www.echoinc.org
Hutoa msaada wa chakula kila mwezi kwa wakazi wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi wa NM wenye mapato yanayostahiki.

**Mradi wa Chakula wa Rio Grande (Rio Grande Food Project)** ……………………………505-831-3778
600 Coors Blvd., NW, 87121 www.rgfp.org

Hutoa msaada wa bidhaa za chakula kwa familia kila mwezi (unahitaji kuchukua chakula baada ya siku 30 kila wakati).

**Benki ya Chakula ya Roadrunner (Roadrunner Food** Bank)………………………………. 505-349-5340
5840 Office Blvd. NE, 87109 https://www.rrfb.org/
Huwapa watu anwani za shirika za msaada wa chakula.

## Msaada wa Umma wa Jimbo

**Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Kitengo cha Msaada wa Mapato cha Idara ya Huduma za Binadamu ya NM (NM Human Services Department Income Support Division (ISD) Customer Service Center)** 1-800-283-4465
Saa za Kupiga Simu: Jumatatu hadi Ijumaa Saa mbili asubuhi (8:00 A.M.) hadi saa kumi na nusu jioni (4:30 P.M.) **www.state.nm.us** Tuma ombi mtandaoni: www.yes.state.nm.us

MIPANGO YA MSAADA YA ISD:

• Msaada wa Mazishi – Msaada mdogo kwa Wateja wa Medicaid. • Medicaid (ya taasisi na isiyo ya taasisi) – Msaada wa Matibabu kwa wenye mapato yanayosatahiki.

• Mipango ya Akiba ya Medicare – QMB (Qualified Medicare Beneficiaries), SLIMB (Specified Low Income Medicare Beneficiaries), Qualifying Individuals (QI) na Qualified Disabled and Working Individuals (QDWI).

• SNAP (ulijulikana zamani kama vocha za chakula) – Msaada wa chakula kwa waombaji wenye mapato yanayostahiki Tovuti ya Mpango wa SNAP

**MPANGO WA LIHEAP**.......................................................................................... 1-888-523-0051
Husaidia watu na familia zinazostahiki msaada wa gharama za mfumo wa kurekebisha joto nyumbani.

## Nyenzo za Baina ya Tamaduni na Tamaduni Nyingi

**Ofisi ya Usawa na Ujumuishwaji (Office of Equity and Inclusion) ya Jiji la of Albuquerque**
505- 768-4712

1 Civic Plaza, NW, Ghorofa ya 2, Ste., 201, 87102 www.cabq.gov/office-of-equity-inclusion

Hushughulikia tofauti za asili ya watu na kutekeleza usawa kwenye jamii na vipengele vyote.

**Ofisi ya Ushirikishaji wa Jamii ya Waafrika (Office of Black Community Engagement) ya Jiji la Albuquerque** 505- 768-3307

Huunganisha nyenzo za Jiji kwa jamii za Waafrika na kutoa ushawishi wa utunzi wa sera za kuhimiza umoja ili kupaza sauti tofauti za Waafrika ndani ya jiji la Albuquerque.

www.cabq.gov/office-of-equity-inclusion/african-american-affairs

**Ofisi ya Mambo ya Wamarekani Asili (Office of Native American Affairs) ya jiji la Albuquerque** 505-768-4547

Ofisi hii imejitolea kuendeleza sera na miradi ya mipango inayohakikisha usalama na ustawi wa Wamarekani Asili na familia zinazoishi katika jiji la Albuquerque na imejitolea kuunga mkono na kukuzwa kwa mahusiano ya serikali mbalimbali kati ya serikali ya Jiji la Albuquerque na serikali za kikabila.

https://www.cabq.gov/office-of-equity-inclusion/about-office-of-equity-inclusion/native-american-affairs

**Kituo cha Jamii ya Waeshia NM (NM Asian Family Center)** ……………………………….505-717-2877

Hutoa huduma za usimamizi wa hali kama vile kutuma maombi ya vocha za chakula, TANF, ustawi wa jamii, nyumba, nk. Huduma zote zinazotolewa zinatolewa bila malipo. Ingawa huduma zetu zinapatikana kwa kila mtu, huduma zetu zinafaa kwa mtu anayejitambulisha kama Mueshia, Mkazi wa Kisiwa cha Pasifiki na Mwenyeji wa Hawaii (APINH). www.nmafc.org

**Shirika la Afuganistani la New Mexico (Afghan Society of New Mexico)**:

Shirika la eneo lisilo la faida ambalo husaidia wahamiaji na wakimbizi wa Afuganistani

Tovuti: Afghan Society of New Mexico

**Kituo cha Waislamu cha New Mexico (Islamic Center of New Mexico):**

Hutoa huduma za dini, jamii na elimu kwa Waislamu katika jiji la Albuquerque na jamii za karibu. Tovuti: http://icnmabq.com/ Nambari ya simu: 505-256-1450

**Kituo cha Jamii cha Waislamu cha Minara cha Jiji la Albuquerque (Minara Muslim Community Center of Albuquerque)**

Shirika la dini lililoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 501(c)3 ambalo limejitolea kuhudumia jamii ya jiji la Albuquerque katika sekta za Kulisha Wasio na Makao (Homeless Feeding), Wito wa Kukubali Uislamu (Islamic Da'wah), Afya na Ustawi (Health & Wellness), Sanaa za Lugha na Kuandika Vizuri (Language Arts & Calligraphy), Sanaa za Kijeshi (Martial Arts (Judo)) na Mafunzo ya Kupiga Mishale (Archery Classes). Nambari ya simu: (505) 440-8036 Facebook: https://www.facebook.com/MinaraABQ/

**Kituo cha Mahdavi cha New Mexico (Mahdavi Center of New Mexico)**

Shirika la dini. Nambari ya simu: (505) 582- 8909

https://www.facebook.com/mahdavi.center2005/about/?ref=page_internal

### Kituo cha Jamii cha Waislamu cha Lighthouse cha New Mexico (The Lighthouse of New Mexico Muslim Community Center)

The Lighthouse of New Mexico, Inc. ni shirika lisilo la faida la Kiislamu.

Tovuti: https://www.thelighthousenm.org/ Nambari ya simu: 505-750-7806

### Kituo cha Kiislamu cha Albuquerque (Albuquerque Islamic Center)

Lengo kuu la AIC ni kutoa huduma za dini, elimu na jamii, kulingana na mafunzo na desturi za Uislamu katika kituo chote cha Kiislamu (Msikiti).

Tovuti: https://www.abqislamiccenter.org/ Nambari ya simu: (505) 299-2579

## Mafunzo ya Kazi na Kuajiriwa

### Idara ya Huduma za Ajira ya NM (NM Department of Workforce Solutions)

501 Mountain Rd NE 87103, Nambari ya simu: 505-843-1900, Jumatatu hadi Ijumaa: Asubuhi hadi Jioni

Tovuti ya NM workforce solutions

### Kituo cha Mpango wa Job Corps cha Albuquerque (Albuquerque Job Corps Center)

Mafunzo ya kiufundi ya elimu na kazi ya bila malipo kwa watu wenye umri wa miaka 16 hadi 24. 500 Indian School Road NW 87104, Nambari ya simu: (505) 222-4243. Tovuti ya Job corps

### Excel Staffing

1700 Louisiana NE, Ste.210 87110, Nambari ya simu: (505) 262-1871

Excel Staffing

# Elimu

**Elimu ya Shule ya Chekechea hadi Darasa la 12 (K-12) – Shule za Umma za Albuquerque (APS, Albuquerque Public Schools)**

Kitengo cha Usimamizi wa Shule cha eneo.**https://www.aps.edu/** Nambari ya simu: 505- 880-3700

**Mpango wa Wakimbizi na Wageni wa APS (APS Refugee and Newcomers Program)**

Kuwapa msaada wanafunzi wakimbizi, familia na shule zinazowahudumia.

Tovuti: Refugee and Newcommers ProgramNambari ya simu: 505- 803-7781

**Chuo cha Jamii cha Eneo la Kati la New Mexico (Central New Mexico Community College (CNM))**505-224-3000

**Kampasi Kuu:** 900 University Blvd. SE, 87106 **www.cnm.edu**

Hutoa mafunzo ya kazi na biashara na mafunzo maalum ya ajira.

**G.E.D, Elimu ya Msingi ya Watu Wazima na Kiingereza kama Lugha ya Pili**

Unahitaji kuwa na kitambulisho cha serikali na ada ya kutuma maombi ya Dola 10 ($10) 505-224-4282

**www.cnm.edu/programs-of-study/programs-a-z/adult-basic-education**

**Idara ya Masuala ya Wazee ya Jiji la Albuquerque (City of Albuquerque Department of Senior Affairs (DSA))** ……………………………………………………………………………………………………505-764-6400

Hutoa mafunzo mbalimbali ikijumuisha mafunzo ya kompyuta, lugha, fasihi/kuandika, sanaa, densi, drama na zaidi kwa watu wenye umri wa miaka 50 na zaidi. Wasiliana na vituo binafsi vya wazee kwa maelezo zaidi.

**www.cabq.gov/seniors**

**Valley Community Interpreters – Chuo cha VCI**……………………………………………(505) 596-0592

Chuo cha VCI hutoa mafunzo ya ukalimani na kinakuza jopokazi la wakalimani katika jimbo la New Mexico ambalo lina ujuzi katika mawasiliano ya jamii mbalimbali ili kuwezesha uelewanaji kati ya watoa huduma na watumaiji wa huduma ambao hawazungumzi lugha sawa. Kozi zote zinafunzwa kwa Kiingereza kwa kutumia mitaala ya kimataifa inayotambulika ya Mawasiliano ya Jamii Mbalimbali inayopatikana mtandaoni au kituoni panapowezekana.
https://www.vcinm.org/vci-academy/

### Encuentro NM

Encuentro hushirikiana na jamii za wahamiaji wa Kilatino katika fursa za elimu na ukuzaji wa taaluma ambazo hukuza ujuzi wa haki ya kiuchumi na kijamii. Kwa mfano:

- ESL (Beginning, Intermediate, Advanced)
- Mafunzo ya Kompyuta
- Uraia
- Elimu ya Fedha
- Maelezo ya Msingi Kuhusu Biashara Ndogo
- Mafunzo ya Mtoa Huduma ya Afya ya Nyumbani kwa Kihispania

Tovuti:https://encuentronm.org/home/ Nambari ya simu: 505- 247 -2920

Anwani: 714 4TH ST SW, Albuquerque, NM 87102

### Chuo cha Salam (Salam Academy)

Chuo cha Salam ni taasisi ya mafunzo yanayolenga kudumisha misingi ya jamii na maadili mema ya wanafunzi Waislamu. Shule hii ihukuza raia kwa mfano wa Marekani ambao ni viongozi wa kipekee katika sekta za sayansi, hisabati na masomo ya jamii. Anwani: 8015 Mountain Road Place NE, Albuquerque, NM 87110 Nambari ya simu: +1 505-888-7688 Tovuti: https://www.salamacademy.org/

### Vizionz Sankofa

Shirika hili hufunza, kukuza na kuwezesha vijana Waafrika na watu wenye umri wa makamo na vijana wengine wa jamii na asili mbalimbali kuhusu kuwa wasimamizi wa maisha yao. Shirika hili hutoa pia mipango ya mafunzo na ushauri.

Anwani: 1258 Ortiz Drive SE, Albuquerque, NM 87108 Nambari ya simu: 505- 506-1604

### Maktaba za Umma za Albuquerque

Maktaba za Albuquerque zina vitabu vya kusikiliza na programu za kompyuta ambazo unaweza kutumia bila malipo ili kujifunza Kiingereza. https://abqlibrary.org/home

Huduma za kuomba usafiri wa maktaba na hati nyingine zinapatikana kwa lugha nyingi katika International District Library.

### Mwongozo wa Nyenzo wa Mtandaoni kwa Wanafunzi wa Chuo wa ESL

https://www.edumed.org/resources/esl-ell-college-students/

**Kituo cha Nyenzo za Wahamiaji na Wakimbizi cha Albuquerque (Immigrant and Refugee Resource Village of Albuquerque (IRRVA)) na Mipango ya Jumla ya Wanawake ya New Mexico (New Mexico Women's Global Pathways)**

IRRVA husaidia watu binafsi na familia kufikia mipango ya Safety-net ambayo huendeleza ustawi wa mtu binafsi na familia na hali ya kujitosheleza kiuchumi ikijumuisha: mafunzo, ushauri, usimamizi wa hali, mafunzo ya kazi na zaidi. Tovuti: https://irrva.com/

Anwani: 120 Mesilla Street NE, Albuquerque, NM, 87108, USA Nambari ya simu: 505-435-5741

## Nyenzo za Ugonjwa wa Virusi vya Korona

**Nambari ya Huduma ya Dharura ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona** 1-855-600-3453

Nambari ya huduma ya dharura kwa wakazi wenye maswali yanayohusiana na afya.

**Nambari ya Huduma ya Dharura ya Maelezo ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona**
1-833-551-0518

Nambari ya huduma ya dharura kwa wakazi wenye maswali yasiyohusiana na afya.
www.newmexico.gov/hotlines

Mradi wa Elimu ya Afya wa Albuquerque

Chati ya kugeuza ni zana ya elimu inayotumiwa na CHW duniani kote. Chati hii ya kugeuza iliundwa ili kusaidia Watoa Huduma ya Afya ya Jamii (Community Heatlh Workers) na washirika wengine wa jamii ili kushiriki habari za kweli kuhusu chanjo, kushughulikia masuala na habari zisizo za kweli kuhusu chanjo, kuelimisha kuhusu vibadala vya ugonjwa wa COVID na kukomesha habari za uongo. Nenda kwenye tovuti hii ili upate chati ya kugeuza kwa lugha nyingi: https://getthefacts.vaccinenm.org/chw/

## Nyenzo za Msaada wa Dharura wa Kodi ya Nyumba

Wakodishaji wa nyumba katika jimbo la New Mexico wanaohitaji msaada wa kulipa kodi na huduma za matumizi au mkopo wa nyumba 833-485-1334

Kutuma Maombi ya Mtandaoni ya Mpango wa Msaada wa Dharura wa Kodi ya Nyumba kwa Kiingereza na Kihispania

**Uhamasisho wa Mahakama wa Mpango wa Msaada wa Kodi ya Nyumba (CORA, Outreach for Rental Assistance Program)** 505-768-3896

Hufanya kazi kwa ushirikiano na Mpango wa Msaada wa Kodi ya Nyumba wa New Mexico (ERAP, New Mexico Emergency Rental Assistance Program) na mfumo wa Mahakama ya Jiji ya Wilaya ya Bernalillo (Bernalillo County Metropolitan Court). Wawakilishi wanaweza kusaidia kufungua akaunti ya mtandaoni, kupiga picha na kupakia hati na kutuma maombi.

## Nyenzo za Ziada

Albuquerque ni Jiji bora la kuishi, kufanya kazi na  burudani. Bila shaka tunakukaribisha katika Jiji letu na tunatumaini kuwa nyenzo tulizoshiriki zinaweza kukusaidia wewe na familia yako. Hata hivyo, tunafahamu kuwa kuna nyenzo nyingine nyingi zinazopatikana ambazo hazijaelezwa katika mwongozo huu.

Tafadhali piga simu kwa nambari 311 wakati unatafuta maelezo au huduma. Unaweza kuomba huduma ya ukalimani kwa njia simu kwa mhudumu. Kwa kufanya hivyo, hakutakuwa na kikwazo cha lugha wakati unaomba maelezo unayotafuta.